JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MADINI

Telegrams "MADINI"
Simu: +255 26230051
Nukushi: +255 262322282
Barua pepe: ps@madini.go.tz

Barabara ya Kikuyu,
S.L.P 422,
40474DODOMA.

YAH: **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI TAREHE 21 NOVEMBA 2018**

Ndugu waandishi wa habari kama mnavyofahamu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika ziara yake mkoani Mara mnamo tarehe 04 hadi 08 Septemba 2018 pamoja na mambo mengine alielekeza kufanyika uchunguzi wa Mfuko wa *North Mara Community Trust Fund* baada ya baadhi ya wananchi wa Nyamongo wilayani Tarime kulalamika juu ya jamii kutofaidika na mfuko huo na badala yake unafaidisha baadhi ya watu wachache.

Ndugu waandishi wa habari, kufuatia maelekezo ya Mhe. Rais kamati ya uchunguzi iliyoundwa na Wizara ya Madini imebaini mambo yafuatayo:-

1. Kati ya Mwaka 1990 hadi 1995, Vijiji vya Nyangoto, Kerende, Kewanja, Genkuru, na Nyamwaga viliwahi kumiliki leseni tano za uchimbaji (CTs). Mwaka 1996, vijiji hivyo vilibadili leseni hizo kwa hiyari yao na kuwa leseni ya utafiti PL 370/96 na kisha kuihamishia kwa Kampuni ya *East African Gold Mining Ltd* (EAGM) na kisha kubadilishwa kuwa leseni ya uchimbaji wa Kati (ML 17/96);

2. Mwaka 1995, Kampuni ya *Keng'anya Enterprises Ltd* (KEL) iliomba na kupata leseni ya utafiti PL 303/95 na kisha kuihamishia leseni hiyo kwa Kampuni ya EAGM kwa hiari yake;
3. Moja ya masharti wakati wa kuhamisha umiliki wa leseni hizo ilikuwa vijiji na Kampuni ya KEL vitakuwa vinapata asilimia moja ya uzalishaji wa dhahabu katika maeneo ya leseni zao;
4. *North Mara Community Trust Fund* ilianzishwa kwa makubaliano kati ya Mgodi na Kampuni ya KEL ya Mwaka 2004. Mfuko huo ulisajiliwa Mwaka 2012 na kuanza kazi Mwaka 2013. Wachangiaji pekee wa Mfuko huo ni KEL na Mgodi kwa kiwango sawa cha asilimia 0.1 ya uzalishaji katika eneo la KEL;
5. Mfuko huu unaendeshwa na wajumbe wa bodi inayoundwa na pande zote tatu yaani Mgodi, KEL na Vijiji, bodi inatakiwa kuwa na wajumbe wasiopungua watano;
6. Shughuli za utendaji zinasimamiwa na menejimenti chini ya meneja wa mfuko, Meneja wa mfuko ndiye msimamizi mkuu wa utendaji wa kila siku wa mfuko pia ni Mtunza Hazina na Katibu wa Bodi ya Wadhamini;
7. Malengo ya kuanzishwa kwa mfuko ni pamoja na kutafuta shughuli zenye manufaa kwa jamii, kuhamasisha, kusaidia na kuwezesha programu na shughuli kwenye maeneo ya elimu, mafunzo, afya, kujenga uwezo, kilimo, maji na kupunguza umasikini kwa ujumla kwa kadri Wadhamini watakavyoona inafaa;
8. Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini wamekuwa wakikopeshwa fedha za Mfuko kinyume na malengo ya uanzishwaji wa mfuko huo;

9. Mwaka 2017 Mfuko ulifungua Kampuni Tanzu (*North Mara Commercial Business Ltd*) ambayo wanahisa wake ni *North Mara Community Trust Fund* (99%) na Bw. Robin Motengi Marwa (1%);

10. Tarehe 14 Mei 2017, Kampuni Tanzu iliingia mkataba na Katoma *Motor Factors Ltd* wa kusambaza mabomba katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita na kuunda Kampuni ya Katoma North Mara Limited ambapo Kampuni Tanzu ilikuwa na asilimia 70 na Katoma asilimia 30 ya hisa, Makubaliano haya hayakuwa na tija kwa mfuko; na

11. Tarehe 20 Aprili 2017, Kampuni tanzu ilitoa kiasi cha Tsh 214,000,000.00 kwenda kwa DAS Tarime kwa ajili ya uwekezaji cha kilimo cha miwa. Fedha hizi zilitolewa kutokana na maombi yaliyowasilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Tarime. Hata hivyo, matumizi ya fedha hizi hayakuzingatia taratibu fedha za umma na manunuzi;

Ndugu waandishi wa habari, kufuatia uchunguzi wa kamati hiyo na yaliyobainika hapo juu, imeamuriwa ifuatavyo:-

1. Kwa kuwa KEL iliomba na kupata PL 303/95 kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia Sekta ya Madini, hivyo malipo ya mrabaha wa asilimia moja yanayopokelewa kutoka kwenye Mgodi kwa mujibu wa mkataba wake ni halali. Hivyo basi, namuagiza Mkuu wa Wilaya ya Tarime aruhusu fedha za KEL kuendelea kulipwa hadi hapo vyombo vya uchunguzi vitakapobaini na kuelekeza vinginevyo. Mkuu wa Mkoa wa MARA asimamie utekelezaji wa agizo hili;

2. Naiagiza TAKUKURU kuchunguza na kuwachukulia hatua za kisheria watumishi wote watakaothibitika kufanya ufujaji na ubadhirifu wa fedha za umma (TSh. 214,000,000.00);

3. Naiagiza TAKUKURU kuwachunguza na kuwachukulia hatua za kisheria wajumbe wa bodi ya wadhamini, menejimenti ya mfuko na mtu mwingine yeyote atakayethibitika kujihusisha na ufujaji na matumizi mabaya ya fedha za mfuko;
4. Naiagiza Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kuvunja uongozi wa Mfuko wa udhamini wa North Mara (Bodi ya Wadhamini na Menejimenti) kwa kuwa umeshindwa kusimamia uendeshaji wa Mfuko kwa tija na kuandaa utaratibu mzuri wa usimamizi wa Mfuko huo ambao utakuwa na manufaa kwa Taifa; na
5. Naiagiza Serikali ya Mkoa kukaa na wamiliki wote wa leseni zilizopo ndani ya Mgodi ambao wanalipwa mrabaha wa asilimia moja kuangalia mfumo bora ili nao wachangie kwenye Mfuko sehemu ya fedha wanazopokea kwa ajili ya maendeleo ya vijiji vinavyozunguka Mgodi wa North Mara.

Imetolewa Mkoani MARA na:

Angellah J. Kairuki (Mb.)
WAZIRI WA MADINI